**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME YA MABADILIKO YA KATIBA**

# MUONGOZO KUHUSU MUUNDO, UTARATIBU WA KUWAPATA WAJUMBE WA MABARAZA YA KATIBA YA WILAYA (MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA) NA UENDESHAJI WAKE

## 1.0. UTANGULIZI

Kwa mujibu wa Kifungu cha 18 (3) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Sura ya 83, Tume inawajibu wa kuunda Mabaraza ya Katiba kwa ajili ya kupitia na kutoa maoni juu ya Rasimu ya Katiba iliyoandaliwa na Tume. Muundo wa Mabaraza ya Katiba unapaswa kuzingatia mgawanyiko wa kijiografia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mabaraza ya Katiba yatawashirikisha na kuwakutanisha wawakilishi kutoka makundi mbalimbali ya wananchi katika jamii kwa lengo la kutoa maoni juu ya Rasimu ya Katiba. Aidha, kifungu cha 17 (8) kinaeleza kuwa, isipokuwa kama mazingira yatahitaji vinginevyo, Tume itabuni utaratibu unaofanana ambao utatumika kila upande wa Muungano.

Kifungu cha 18 (6) kinaeleza aina nyingine ya Mabaraza ya Katiba kwa kueleza kuwa Tume inaweza kuruhusu Asasi, Taasisi au Makundi ya Watu kuwasilisha maoni yao kuhusu Rasimu ya Katiba.

Kwa Msingi huo, Tume imeamua kuwa Mabaraza ya Katiba yatakuwa katika makundi mawili yafuatayo:-

1.1 Mabaraza ambayo Tume itayasimamia na kukusanya Maoni **(Mabaraza ya Katiba ya Wilaya – Ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa).**

1.2 Mabaraza ambayo Tume haitayasimamia. Mabaraza hayo yatajisimamia yenyewe na kukusanya maoni yatakayowasilishwa kwenye Tume kwa mujibu wa maelekezo. **(Mabaraza ya Katiba ya Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu).**

Muongozo huu unaainisha Muundo, Utaratibu wa kuwapata Wajumbe na Utaratibu wa Uendeshaji wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yatakayoendeshwa na kusimamiwa na Tume.

## 2.0. MABARAZA YA KATIBA YA WILAYA NGAZI YA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

Kwa kuzingatia mgawanyiko wa kijiografia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mabaraza ya Katiba ya Wilaya – Ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yataundwa kwenye kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika ngazi ya Halmashauri za Jiji, Manispaa, Mji, Wilaya na Mabaraza ya Miji.

**Kwa upande wa Tanzania Bara**, Katika Mikoa yote ngazi ya kupata wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya (Mamlaka za Serikali za Mitaa) itakuwa ni Ngazi ya Kata. Wajumbe watapigiwa kura za kupendekezwa kwenye ngazi za Kijiji/Mitaa na kuchaguliwa kwenye ngazi ya Kata.

**Kwa upande wa Zanzibar**, Katika Mikoa yote ngazi ya kupata wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya (Mamlaka za Serikali za Mitaa) itakuwa ni Shehia. Wajumbe watapigiwa kura kwenye ngazi za Shehia.

Muundo na utaratibu huu umezingatia changamoto mbalimbali zikiwemo; ukubwa wa Mabaraza ya Katiba, utaratibu wa kuwapata wajumbe, ufanisi katika uendeshaji wa Mabaraza ya Katiba, gharama ya kufanikisha shughuli ya Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, na tofauti ya Mfumo wa Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Zanzibar.

Kutokana na changamoto hizo, utaratibu wa kuwapata wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya haufanani kwa pande zote za Muungano.

## 3.0. WAJUMBE WA MABARAZA YA KATIBA YA WILAYA NGAZI YA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

### 3.1. Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba.

Mabaraza ya Katiba katika ngazi ya Halmashauri za Jiji, Manispaa, Mji, Wilaya na Mabaraza ya Miji yataundwa na Wajumbe wafuatao:

3.1.1. **Kwa Tanzania Bara.**

3.1.1.1 Wajumbe wanne kutoka kila Kata watachaguliwa kwa utaratibu utakaofafanuliwa na Muongozo huu.

3.1.1.2 Wajumbe wanane kutoka kila Kata kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

3.1.2. **Kwa Zanzibar.**

3.1.2.1. Wajumbe watatu kutoka kila Shehia watachaguliwa kwa utaratibu utakaofafanuliwa na Muongozo huu.

3.1.3. **Kwa pande zote za Muungano.**

3.1.3.1. Madiwani wa kuchaguliwa kwenye Kata / Wadi.

3.1.3.2. Madiwani wa Viti Maalum.

3.1.3.3. Madiwani wa kuteuliwa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa kwa pande zote za Muungano, [Madiwani waliopo kazini kwa sasa].

## 3.2. Ngazi ya Msingi ya kuwapata Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba

3.2.1. **Kwa upande wa Tanzania Bara**

Kwa Mikoa yote ya Tanzania Bara, ngazi ya msingi ya kuwapata wajumbe wa Mabaraza ya Katiba itakuwa Kata.

3.2.2. **Kwa upande wa Zanzibar**

Kwa Mikoa yote ya Zanzibar, ngazi ya msingi ya kuwapata wajumbe wa Mabaraza ya Katiba itakuwa Shehia.

## 3.3. Idadi ya Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Idadi ya wajumbe itakuwa kama ifuatavyo:

3.3.1. **Kwa Tanzania Bara**, idadi ya Mabaraza ya Katiba yatakayoendeshwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ni **163** ambapo kila Mamlaka moja ya Serikali za Mitaa ngazi ya Wilaya itakuwa na Baraza moja la Katiba ukiondoa Mkoa wa Dar es Salaam ambapo kila Halmashauri itakuwa na Mabaraza mawili ya Katiba. Hivyo, jumla ya Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa itakuwa **163 (zipo Mamlaka za Serikali za Mitaa 160)**.

3.3.2. Katika Mikoa **24** ya Tanzania Bara, kila kata itawakilishwa na Wajumbe wanne (**4**) ambao wataungana na Madiwani wa Kata na Viti Maalum. Idadi ya Kata ni **3,339** ukiondoa kata **90** za Mkoa wa Dar es Salaam, zinabaki kata **3,249** [utaratibu wa kuwapata wajumbe kwa Mkoa wa Dar es Salaam ni tofauti na Mikoa mingine ya Tanzania Bara na umefafanuliwa katika aya ya 3.3.3]. Hivyo, Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya kutoka kwenye Kata zote isipokuwa kata 90 za Mkoa wa Dar es Salaam, watakuwa **12,996** na idadi ya Madiwani wote ni **4,453**.

3.3.3. Kwa Mkoa wa Dar es Salaam, wenye Kata **90** utawakilishwa na Wajumbe wanane **(8)** kutoka kila Kata. Kwa hiyo, idadi ya Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya kutoka Mkoa Dar es Salaam watakuwa **720** watakaoungana na wajumbe wengine kama ilivyofafanuliwa kwenye aya ya 3.3.2.

Hivyo, Jumla ya wajumbe wote wa Mabaraza ya Katiba kwa Tanzania Bara watakuwa **18,169** kwa mchanganuo ufuatao:-

| | |
|---|---|
| 3.3.3.1. Idadi ya Wajumbe 4 kutoka kila Kata | **12,996** |
| 3.3.3.2. Idadi ya Wajumbe 8 kutoka Kata za Mkoa wa Dar es salaam | **720** |
| 3.3.3.3. Idadi ya Madiwani wote ni: | **4,453** |
| **JUMLA:** | **18,169** |

3.3.4. **Kwa upande wa Zanzibar,** idadi ya Mabaraza ya Katiba yatakayoendeshwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ni **13** ambapo kila Mamlaka moja ya Serikali za Mitaa itakuwa na Baraza moja la Katiba (**zipo Mamlaka za Serikali za Mitaa 13**).

3.3.5. Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 13 za Zanzibar, kila Shehia itawakilishwa na Wajumbe watatu (**3**) ambao wataungana na Madiwani wa Wadi, Viti Maalum, na Wakuteuliwa waliopo kazini kwa sasa. Idadi ya Shehia ni **335.** Hivyo, Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya kutoka kwenye Shehia zote watakuwa **1,005** na idadi ya Madiwani wote ni **193**.

Hivyo, Jumla ya wajumbe wote wa Mabaraza ya Katiba kwa Zanzibar watakuwa **1,198** kwa mchanganuo ufuatao:-

| | |
|---|---|
| 3.3.5.1. Idadi ya Wajumbe kutoka kila Shehia: | **1,005** |
| 3.3.5.2. Idadi ya Madiwani Wote ni: | **193** |
| **JUMLA** | **1,198** |

Mchanganuo wa idadi ya wajumbe kwa kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni kama ilivyo kwenye **Jedwali "1"** kwa upande wa Tanzania Bara na **Jedwali "2"** kwa Zanzibar.

## 4.0. SIFA ZA WATAKAOCHAGULIWA KUWA WAJUMBE WA MABARAZA YA KATIBA YA WILAYA NGAZI YA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA.

Wajumbe wanne kutoka kila Kata kwa Tanzania Bara na wanane kutoka kila Kata katika Mkoa wa Dar es Salaam na Wajumbe watatu kutoka kila Shehia kwa Zanzibar wanapaswa kuwa na sifa zifuatazo:

**4.1.** Awe Raia wa Tanzania.

**4.2.** Awe na umri wa miaka 18 au zaidi.

**4.3.** Awe na uwezo wa kusoma na kuandika.

**4.4.** Awe mkazi wa kudumu wa Kijiji/ Mtaa / Shehia husika.

**4.5.** Awe Mtu mwenye hekima, busara na uadilifu.

**4.6.** Awe Mtu mwenye uwezo wa kujieleza na kupambanua mambo.

## 5.0. MAMBO YA KUZINGATIWA

Utaratibu wa kuwapata Wajumbe kwa Tanzania Bara na Zanzibar uzingatie mambo yafuatayo:-

**5.1.** Uwakilishi wa watu wazima.

**5.2.** Uwakilishi wa wanawake.

**5.3.** Uwakilishi wa vijana.

**5.4.** Jiografia ya Kata/ Wadi / Kijiji / Mtaa / Shehia husika.

## 6.0. UTARATIBU WA KUWAPATA WAJUMBE KWENYE MABARAZA YA KATIBA YA WILAYA NGAZI YA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

### 6.1. Kwa upande wa Tanzania Bara utaratibu utakuwa kama ifuatavyo:

**Kwa Mikoa yote isipokuwa Mkoa wa Dar es Salaam.**

6.1.1. Kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa kwenye aya za 4.0 na 5.0, kila Mwananchi wa Kijiji / Mtaa husika anayependa kuwa mjumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa atawasilisha jina lake kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji / Mtaa. Uwasilishaji huo uambatane na taarifa zifuatazo:

6.1.1.1. Majina kamili ya mwombaji.

6.1.1.2. Jinsi yake.

6.1.1.3. Umri wake.

6.1.1.4. Elimu yake.

6.1.1.5. Kazi yake.

6.1.1.6. Sehemu anayoishi katika Kijiji / Mtaa husika.

6.1.2. Orodha ya majina ya Wananchi wote wanaotaka kuwa Wajumbe yatabandikwa kwenye maeneo ya wazi / matangazo ya kila Ofisi za Kijiji / Mtaa siku saba (7) kabla ya Mkutano ili wananchi wapate fursa ya kuyapitia na kujiridhisha kama walioomba wana sifa zilizoanishwa kwenye aya za 4.0 na 5.0.

6.1.3. Afisa Mtendaji wa Kijiji / Mtaa ataitisha Mkutano Mkuu wa Kijiji / Mtaa ambao utakuwa na agenda moja tu ya kuwapendekeza kwa kuwapigia kura watu wanne ambao majina yao yatawasilishwa kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata. Mkutano huu utaendeshwa na Mwenyekiti wa Kijiji / Mtaa, ambapo Afisa Mtendaji wa Kijiji / Mtaa atakuwa Katibu wa Mkutano huo na ndiye atakayewasilisha majina ya wananchi wote walioomba kuingia kwenye Baraza la Katiba la Wilaya.

6.1.4. Kwa kuzingatia Sifa zilizoainishwa katika aya za 4.0. na 5.0, Mkutano Mkuu wa Kijiji / Mtaa utayapigia kura ya siri majina ya wananchi walioomba kuwa Wajumbe wa Baraza la Katiba la Wilaya ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

6.1.5. Utaratibu wa kupiga kura za kwenye Mkutano Mkuu Maalum wa kuwachagua Wananchi wanne wanaopendekezwa kuwa Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya utakuwa kama ifuatavyo:

6.1.5.1. Kwanza, Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji / Mtaa watapiga kura ya siri ya kumchagua **Mtu mzima mmoja** [anaweza kuwa mwanamke au mwanaume].

6.1.5.2. Pili, Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji / Mtaa watapiga kura ya siri kumchagua **Mwanamke mmoja**.

6.1.5.3. Tatu, Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji / Mtaa watapiga kura ya siri kumchagua **Kijana mmoja** [anaweza kuwa Mwanaume au Mwanamke].

6.1.5.4. Nne, Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji / Mtaa watapiga kura ya siri kumchagua **Mtu mwingine yeyote.**

6.1.6. Orodha ya majina ya wananchi wanne waliopigiwa kura nyingi za kupendekezwa kuwa Wajumbe wa Baraza la Katiba la Wilaya ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, yatabandikwa kwenye maeneo ya wazi/ matangazo ya kila Ofisi ya Serikali ya Kijiji / Mtaa.

6.1.7. Majina ya watu wanne yatakayokuwa yamepata kura nyingi kuliko mengine yatawasilishwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji / Mtaa kwa Afisa Mtendaji wa Kata yakiwa yameambatanishwa na Muhtasari wa

Mkutano Mkuu Maalum wa Kijiji / Mtaa uliosainiwa na Mwenyekiti wa Kijiji /Mtaa pamoja na orodha ya wananchi waliohudhuria.

6.1.8. Afisa Mtendaji wa Kata baada ya kupokea majina yaliyopendekezwa kutoka kwenye Mikutano Mikuu Maalum ya Vijiji / Mitaa ya Kata husika, ataitisha Kikao Maalum cha Kamati ya Maendeleo ya Kata, ambacho kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa kwenye aya za 4.0 na 5.0 kitachagua majina manne kwa kura ya siri kwa utaratibu ufuatao:

6.1.8.1. Kwanza, Wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Kata watapigia kura ya siri ya kumchagua **Mtu mzima mmoja** [anaweza kuwa mwanamke au mwanaume].

6.1.8.2. Pili, Wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Kata watapiga kura ya siri kumchagua **Mwanamke mmoja**.

6.1.8.3. Tatu, Wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Kata watapiga kura ya siri kumchagua **Kijana mmoja** [anaweza kuwa Mwanaume au Mwanamke].

6.1.8.4. Nne, Wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Kata watapiga kura ya siri kumchagua **Mtu mwingine yeyote.**

6.1.9. Jina la Mwananchi atakayekuwa amepata kura nyingi kutoka kila kundi **[Mtu mzima, Mwanamke, Kijana na Mtu mwingine]** yatawasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa yakiwa na Muhtasari uliosainiwa na Mwenyekiti na Katibu wa Kikao Maalum cha Kamati ya Maendeleo ya Kata kilichoyapigia kura majina hayo pamoja na orodha ya wajumbe waliohudhuria.

6.1.10. Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kuzingatia sifa na utaratibu ulioainishwa kwenye aya ya 4.0 na 5.0, atawasilisha majina kwa Katibu wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa Uteuzi.

6.1.11. Endapo Diwani wa kata ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Kata hatakuwepo [Kwa sababu zozote ikiwa ni pamoja na kuwa safarini kwa kipindi ambacho Mabaraza ya Katiba yatafanyika, kuwa mgonjwa na kutoweza kutekeleza majukumu ya Udiwani, Kifo au sababu nyingine], utaratibu wa kawaida wa kumpata mwenyekiti wa kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Kata wakati diwani hayupo utatumika, ambapo Mwenyekiti wa Kijiji atakayependekezwa na Wajumbe wenzake wa Kamati ya Maendeleo ya Kata kuendesha Kikao hicho ndiye atawakilisha kata badala ya Diwani.

**6.2. Kwa Mkoa wa Dar es Salaam utaratibu utakuwa kama ifuatavyo:**

6.2.1. Kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa kwenye aya za 4.0 na 5.0, kila Mwananchi wa Mtaa husika anayependa kuwa mjumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa atawasilisha jina lake kwa Afisa Mtendaji wa Mtaa. Uwasilishaji huo uambatane na taarifa zifuatazo:

6.2.1.1. Majina kamili ya mwombaji.

6.2.1.2. Jinsi yake.

6.2.1.3. Umri wake.

6.2.1.4. Elimu yake.

6.2.1.5. Kazi yake.

6.2.1.6. Sehemu anayoishi katika Kata husika.

6.2.2. Orodha ya majina ya Wananchi wote wanaotaka kuwa wajumbe wa Baraza la Katiba la Wilaya ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, itawekwa kwenye maeneo ya wazi / matangazo ya Ofisi za Mtaa kwa siku saba (7) kabla ya Mkutano ili wananchi wa Mtaa husika wapate fursa ya kuyapitia na kujiridhisha kama walioomba wana sifa zilizoanishwa kwenye aya za 4.0 na 5.0.

6.2.3. Afisa Mtendaji wa Mtaa ataitisha Mkutano Mkuu Maalum wa Mtaa ambao utakuwa na agenda moja tu kuwapendekeza kwa kuwapigia kura ya siri watu Wanane watakaokuwa wajumbe wa Mabaraza ya katiba ya Wilaya ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

6.2.4. Mkutano Mkuu Maalum wa Mtaa wa kuwachagua wananchi wanane **(8)** kuwa Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa utaendeshwa na Mwenyekiti wa Mtaa ambapo Afisa Mtendaji wa Mtaa atakuwa Katibu, na ndiye atakayewasilisha majina ya wananchi wote kwenye Mkutano huo walioomba kuingia kwenye Baraza la Katiba la Wilaya.

6.2.5. Utaratibu wa kupiga kura za kwenye Mkutano Mkuu Maalum wa kuwachagua Wananchi wanane wanaopendekezwa kuwa Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya utakuwa kama ifuatavyo:

6.2.5.1. Kwanza, Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu Maalum wa Mtaa watapiga kura ya siri ya kuwachagua **Watu Wazima Wawili** [wanaweza kuwa Wanawake au Wanaume].

6.2.5.2. Pili, Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu Maalum wa Mtaa watapiga kura ya siri kuwachagua **Wanawake wawili**.

6.2.5.3. Tatu, Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu Maalum wa Mtaa watapiga kura ya siri kuwachagua **Vijana wawili** [wanaweza kuwa Wanaume au Wanawake].

6.2.5.4. Nne, Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu Maalum wa Mtaa watapiga kura za siri kuwachagua **Watu wengine wowote wawili.**

6.2.6. Orodha ya majina ya wananchi wanane waliopigiwa kura nyingi za kupendekezwa kuwa Wajumbe wa Baraza la Katiba la Wilaya ngazi ya

Mamlaka za Serikali za Mitaa, yatabandikwa kwenye maeneo ya wazi/ matangazo ya kila Ofisi ya Serikali ya Mtaa.

6.2.7. Majina ya watu wanane yatakayokuwa yamepata kura nyingi kuliko mengine yatawasilishwa na Afisa Mtendaji wa Mtaa kwa Afisa Mtendaji wa Kata yakiwa yameambatanishwa na Muhtasari wa Mkutano Mkuu Maalum wa Mtaa uliosainiwa na Mwenyekiti wa Mtaa pamoja na orodha ya wananchi waliohudhuria.

6.2.8. Afisa Mtendaji wa Kata baada ya kupokea majina yaliyopendekezwa kutoka kwenye Mikutano Mikuu Maalum ya Mitaa ya Kata husika, ataitisha Kikao Maalum cha Kamati ya Maendeleo ya Kata, ambacho kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa kwenye aya za 4.0 na 5.0 kitachagua majina manane kwa kura ya siri kwa utaratibu ufuatao:

6.2.8.1. Kwanza, Wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Kata watapiga kura ya siri ya kuwachagua **Watu wazima wawili** [wanaweza kuwa Wanawake au Wanaume].

6.2.8.2. Pili, Wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Kata watapiga kura ya siri kuwachagua **Wanawake wawili**.

6.2.8.3. Tatu, Wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Kata watapiga kura ya siri kuwachagua **Vijana wawili** [wanaweza kuwa wanaume au wanawake].

6.2.8.4. Nne, Wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Kata watapiga kura ya siri kuwachagua **watu wengine wowote wawili.**

6.2.9. Majina ya Wananchi watakaokuwa wamepata kura nyingi kutoka kila kundi **[Watu wazima wawili, Wanamke wawili, Vijana wawili**

**na Watu wawili wengine]** yatawasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa yakiwa na Muhtasari uliosainiwa na Mwenyekiti na Katibu wa Kikao Maalum cha Kamati ya Maendeleo ya Kata kilichoyapigia kura majina hayo pamoja na orodha ya wajumbe waliohudhuria.

6.2.10. Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kuzingatia sifa na utaratibu ulioainishwa kwenye aya ya 4.0 na 5.0, atawasilisha majina kwa Katibu wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa Uteuzi.

6.2.11. Endapo Diwani wa kata ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Kata hatakuwepo [Kwa sababu zozote ikiwa ni pamoja na kuwa safarini kwa kipindi ambacho Mabaraza ya Katiba yatafanyika, kuwa mgonjwa na kutoweza kutekeleza majukumu ya Udiwani, Kifo au sababu nyingine], utaratibu wa kawaida wa kumpata mwenyekiti wa kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Kata wakati diwani hayupo utatumika, ambapo Mwenyekiti wa Kijiji atakayependekezwa na Wajumbe wenzake wa Kamati ya Maendeleo ya Kata kuendesha Kikao hicho ndiye atawakilisha kata badala ya Diwani.

**6.3. Kwa upande wa Zanzibar utaratibu utakuwa kama ifuatavyo:**

6.3.1. Kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa kwenye aya za 4.0 na 5.0, kila Mwananchi Mkaazi wa Shehia husika anayependa kuwa mjumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa atawasilisha jina lake kwa Sheha. Uwasilishaji huo uambatane na taarifa zifuatazo:

6.3.1.1. Majina kamili ya mwombaji.
6.3.1.2. Jinsi yake.
6.3.1.3. Umri wake.
6.3.1.4. Elimu yake.

6.3.1.5. Kazi yake.

6.3.1.6. Sehemu anayoishi katika Shehia husika.

6.3.2. Orodha ya majina ya Wananchi wote walioomba kuwa wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yatabandikwa kwenye maeneo ya wazi (mfano Skuli) / matangazo katika Shehia husika siku saba (7) kabla ya Mkutano ili wananchi wapate fursa ya kuyapitia na kujiridhisha kama walioomba wana sifa zilizoanishwa kwenye aya za 4.0 na 5.0.

6.3.3. Sheha ataitisha Mkutano wa Shehia husika ambao utakuwa na agenda moja tu ya kuwapigia kura ya siri watu watatu [3] ambao majina yao yatawasilishwa kwa Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa, Katibu wa Halmashauri Mji/ Wilaya ambapo Shehia hiyo ipo.

6.3.4. Mkutano wa Shehia utachagua Mwenyekiti na Katibu wa Mkutano huo kutoka miongoni mwa wananchi waliohudhuria Mkutano. Katibu ndiye atakayewasilisha kwenye Mkutano majina ya wananchi wote walioomba kuwa Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

6.3.5. Mwenyekiti na Katibu wa Mkutano wa Shehia watakaochaguliwa sharti wawe na sifa kama za Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba zilivyoainishwa katika aya ya 4.0.

6.3.6. Utaratibu wa kupiga kura kwenye Mkutano wa Shehia wa kuwachagua Wananchi watatu kuwa Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya utakuwa kama ifuatavyo:

6.3.6.1. Kwanza, Wananchi wote waliohudhuria Mkutano wa Shehia watapiga kura ya siri ya kumchagua **Mtu mzima mmoja** [anaweza kuwa mwanamke au mwanaume].

6.3.6.2. Pili, Wananchi wote waliohudhuria Mkutano wa Shehia watapiga kura ya siri kumchagua **Mwanamke mmoja**.

6.3.6.3. Tatu, Wananchi wote waliohudhuria Mkutano wa Shehia watapiga kura ya siri kumchagua **Kijana mmoja** [anaweza kuwa Mwanaume au Mwanamke].

6.3.7. Matokeo ya upigaji kura wa siri yatatangazwa kwenye Mkutano baada ya mchakato wa kupiga kura kukamilika na kuwekwa kwenye maeneo ya wazi / matangazo katika Shehia husika.

6.3.8. Katibu wa Mkutano wa Shehia atawasilisha majina ya watu waliochaguliwa katika Mikutano ya Shehia kwa Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa, Katibu wa Halmashauri ya Mji / Wilaya ambapo Shehia hiyo ipo katika muda wa siku moja tangu Mkutano ulipofanyika. Mawasilisho hayo yaambatane na muhtasari wa Mkutano uliotiwa saini na Mwenyekiti na Katibu pamoja na orodha ya majina ya wananchi waliohudhuria.

6.3.9. Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa, Katibu wa Halmashauri Mji/ Wilaya kwa kuzingatiaji sifa na utaratibu ulioainishwa kwenye aya za 4.0 na 5.0, atawasilisha majina kwa Katibu wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa uteuzi.

Katibu wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba baada ya kupokea orodha ya majina ya watu waliochaguliwa kuwa Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka Tanzania Bara na Zanzibar; Katibu au kwa niaba yake kama atakavyoelekeza, atatoa barua rasmi za kuwateua Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

## 7.0. MABARAZA YA KATIBA YA ASASI, TAASISI NA MAKUNDI YA WATU

Kama ilivyoelezwa hapo awali, Kifungu cha 18 (6) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Sura ya 83, kinaeleza aina nyingine ya Mabaraza ya Katiba kwa mujibu wa Kifungu cha 18 (6), Tume inaweza kuruhusu Asasi, Taasisi au Makundi ya Watu kuwasilisha maoni yao kuhusu Rasimu ya Katiba.

Tume inaruhusu Asasi, Taasisi na Makundi ya Watu wenye malengo yanayofanana kuunda Mabaraza ya Katiba yatakayojiendesha yenyewe na kuwasilisha maoni yao katika muda utakaopangwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Orodha hiyo ni pamoja na:

1.1. Jumuiya ya kidini.
1.2. Chama cha siasa.
1.3. Asasi ya kiraia.
1.4. Taasisi ya elimu ya juu.
1.5. Chama cha wafanyakazi.
1.6. Chama cha wakulima.
1.7. Chama cha wafugaji.
1.8. Chama cha Wanahabari.
1.9. Mabaraza ya Watoto, Vijana na Wazee.
1.10. Kundi au makundi ya watu wenye malengo yanayofanana kama Sheria inavyoelekeza, na
1.11. Kundi au makundi ya watu wenye mahitaji maalum katika jamii.

## 8.0. TARATIBU ZA KUFANYA MIKUTANO YA KUWAPATA WAJUMBE WA MABARAZA YA KATIBA YA WILAYA.

Ili kuendana na muda wa kuwapata Wajumbe na kufanyika kwa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na maandalizi yote muhimu, vikao vya kupendekeza majina na kufanya uchaguzi vitafanyika kwa utaratibu ufuatao:

**8.1.** Wananchi wanaopenda kuwa Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya wawasilishe majina yao kwa Maafisa Watendaji wa Vijiji / Mitaa kwa

Tanzania Bara na kwa Sheha kwa Zanzibar katika tarehe itakayoelekezwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

**8.2.** Orodha ya majina ya wananchi wote wanaotaka kuwa Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa iwekwe kwenye maeneo ya wazi / matangazo katika Ofisi za Vijiji / Mitaa kwa Tanzania Bara na katika maeneo ya wazi / matangazo kwenye Shehia husika kwa Zanzibar katika tarehe itakayoelekezwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

**8.3.** **Kwa Tanzania Bara,** Vikao vya Vijiji / Mitaa vya kuwachagua kwa kuwapigia kura za siri wananchi wanne kuwa wajumbe wa Mabaraza ya Katiba vitafanyika katika tarehe itakayoelekezwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

**8.4.** **Kwa upande wa Tanzania Bara,** Kikao Maalum cha Kamati ya Maendeleo ya Kata cha kuwachagua wajumbe wanne kutoka miongoni mwa wananchi waliopigiwa kura na Mikutano Mikuu ya Vijiji / Mitaa kitafanyika katika tarehe itakayoelekezwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

**8.5.** **Kwa Tanzania Bara**, majina ya Wajumbe wanne waliochaguliwa na Kikao Maalum cha Kamati ya Maendeleo ya Kata, yawasilishwe kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika katika tarehe itakayoelekezwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

**8.6.** **Kwa Mkoa ya Dar es salaam**,

8.6.1. Vikao vya Mitaa vya kuwapigia kura ya kuwapendekeza wajumbe wanane wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya vitafanyika katika tarehe itakayoelekezwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

8.6.2. Vikao Maalum vya Kamati za Maendeleo za Kata vya kuwachagua wajumbe wanane kutoka miongoni mwa wananchi waliopigiwa

kura na Mikutano Mikuu ya Mitaa vitafanyika katika tarehe itakayoelekezwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

8.6.3. Majina ya Wajumbe wanane waliochaguliwa na Kikao Maalum cha Kamati ya Maendeleo ya Kata, yawasilishwe kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika kwa tarehe itakayoelekezwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

**8.7.** **Kwa Zanzibar,** Vikao vya Shehia vya kuwachagua kwa kuwapigia kura za siri wananchi watatu kuwa wajumbe wa Mabaraza ya Katiba vitafanyika katika tarehe itakayoelekezwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

**8.8.** **Kwa Zanzibar**, majina ya Wajumbe watatu, waliochaguliwa na Mikutano ya Shehia, yawasilishwe kwa Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa, Katibu wa Halmashauri ya Mji / Wilaya ambapo Shehia hiyo ipo katika tarehe itakayoelekezwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

**8.9.** Majina ya watu wote waliochaguliwa kuwa wajumbe wa Mabaraza ya Katiba, pamoja na majina ya Madiwani wote wa Mamlaka ya Serikali ya Mtaa husika yawasilishwe kwa Katibu wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa kutumia Fomu maalum iliyoandaliwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa madhumuni hayo kwa njia ya nakala tete ***(soft Copy)*** na nakala mango ***(hard copy)*** katika tarehe itakayoelekezwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

## 9.0. MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA MCHAKATO WA KUWAPATA WAJUMBE WA MABARAZA YA KATIBA YA WILAYA

### 9.1. Kwa Tanzania Bara isipokuwa kwa Mkoa wa Dar es Salaam

9.1.1. Ni Jukumu la Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kusimamia, kuratibu na kuhakikisha Mikutano hiyo inafanyika.

9.1.2. Mikutano yote ya Vijiji / Mitaa itaendeshwa na Wenyeviti wa Serikali za Vijiji / Mitaa na Maafisa Watendaji wa Vijiji / Mitaa watakuwa ni Makatibu na wasimamizi wa Mikutano hiyo.

9.1.3. Mikutano Mikuu yote ya Vijiji / Mitaa itakayoitishwa kwa lengo la kuwapigia kura ya siri watu wanne kuwa wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya vitafanyika katika tarehe moja kwenye Vijiji / Mitaa yote iliyopo kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika.

9.1.4. Vikao vyote vya Kamati za Maendeleo ya Kata vitakavyokuwa na jukumu la kuwachagua watu wanne kuwa Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa vitafanyika katika tarehe moja kwenye Kata zote za Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika.

9.1.5. **Kwa Mkoa wa Dar es Salaam:**

9.1.5.1. Mikutano Mikuu yote ya Mitaa itakayoitishwa kwa lengo la kuwapigia kura watu wanane wanaopendekezwa kuwa Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya itafanyika katika tarehe moja kwenye Mitaa yote iliyopo kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika.

9.1.5.2. Vikao vyote vya Kamati za Maendeleo ya Kata vitakavyokuwa na jukumu la kuwachagua watu wanane kuwa Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa vitafanyika katika tarehe moja kwenye Kata zote za Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika.

## 9.2. Kwa Zanzibar

9.2.1. Ni jukumu la Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa, Katibu wa Halmashauri ya Mji / Wilaya kusimamia, kuratibu na kuhakikisha Mikutano hiyo inafanyika.

9.2.2. Mikutano yote ya Shehia itaendeshwa na Wenyeviti na Makatibu watakaochaguliwa na Mikutano hiyo.

9.2.3. Jukumu la Sheha ni:

- 9.2.3.1. Kupokea majina ya wananchi wanaoomba kuwa Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya.
- 9.2.3.2. Kubandika katika maeneo ya wazi / matangazo majina yote ya watu walioomba kuwa wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya.
- 9.2.3.3. Kuitisha Mkutano wa Shehia utakaochagua Mwenyekiti na Katibu wa Mkutano.

9.2.4. Majukumu ya Katibu wa Mkutano atakayechaguliwa:

- 9.2.4.1. Kupokea orodha ya majina ya wananchi wote walioomba kuwa Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya kutoka kwa Sheha.
- 9.2.4.2. Kuwasilisha majina ya wananchi wote walioomba kuwa Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba ya Wilaya kwenye Mkutano.
- 9.2.4.3. Kuratibu mchakato wa uchaguzi kwenye Mkutano.
- 9.2.4.4. Kubandika kwenye maeneo ya wazi / matangazo matokeo ya kura kwa kila mwombaji alivyopata baada ya Mkutano.
- 9.2.4.5. Kuandaa Muhtasari wa Mkutano.
- 9.2.4.6. Kuwasilisha majina ya Wananchi walioshinda pamoja na Muhtasari wa Mkutano kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa iliyopo kwenye Shehia husika.

## 10.0. TAREHE YA KUANZA KUTUMIKA KWA MWONGOZO HUU

Mwongozo huu utaanza kutumika kuanzia tarehe itakayoelekezwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

Tume ya mabadiliko ya katiba inawaomba wananchi wote kupitia mwongozo huu uliotolewa na Tume na kuwasilisha maoni/Mapendekezo yao katika kipindi cha wiki mbili (2) baada ya tarehe ya kutolewa tangazo hili.Maoni hayo yawasilishwe Tume kupitia :


Makao Makuu<br>
Mtaa wa Ohio,S.L.P 1681,<br>
DAR ES SALAAM<br>
Simu:+25522 2133425<br>
Nukushi(Faksi):+255 22 2133442<br>
Tovuti:www.katiba.go.tz

Au

Ofisi Ndogo<br>
Jengo la Ofisi ya Mfuko wa Barabara,<br>
Mtaa wa Kikwajuni Gofu<br>
S.L.P 2775<br>
ZANZIBAR<br>
Simu: +255 224 3220768<br>
Nukushi: +255 224 2230769


Jaji Joseph S. Warioba<br>
**Mwenyekiti**<br>
**Tume ya Mabadiliko ya Katiba**